

Uwezo wa Lugha katika Matini ya Siasa Nchini Kenya Kuanzia Mwaka 2002 hadi 2005. , 2014

Adero, Margan, Carlpeters

Abstract:

Utafiti huu unaangazia uwezo wa lugha katika matini ya siasa nchini Kenya. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kudhihirisha vile lugha hutumiwa na wanasiasa ili waweze kuonyesha itikadi zao na pia kupata mamlaka. Ili kuonyesha uwezo wa lugha katika matini za siasa nadharia ya uchanganuzi usemi hakiki ndio imetumiwa. Katika utafiti huu sura ya kwanza ambayo ni utangulizi wa tasnifu inashughulikia swala la utafiti, sababu za kuchagua mada, nadharia, madhumuni, upeo wa utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada na mbinu za utafiti. Sura ya pili inaangazia na kueleza dhana muhimu zilizotumiwa katika utafiti. Pia inaelezea mwingiliano uliopo kati ya lugha, siasa, mamlaka na itikadi. Sura ya tatu inahusu uchanganuzi wa data ya hotuba za kisiasa na kuzichanganua kimuktadha na kimaana. Inatoa maelezo ya hotuba zilizotolewa katika kipindi cha siasa kinachozungumziwa. Sura ya nne ni uchanganuzi wa data na kueleza uwezo huo wa lugha katika hotuba za kisiasa nchini Kenya. Sura ya tano ni matokeo ya utafiti, mapendekezo ya utafiti mwingine na matatizo yaliyoukumba utafiti.